



Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

KIKAO KAZI CHA 3 CHA SERIKALI MTANDAO 2023

Ndugu Wanahabari,

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inatarajia kufanya Kikao Kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kuanzia Februari **8-10, 2023** katika Ukumbi wa AICC – jijini Arusha. Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora **Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb).**

Takriban wadau **1000** wa Serikali Mtandao kutoka katika Mashirika na Taasisi za Umma wakiwemo Maafisa Masuuli, Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Vitengo vyta TEHAMA, Maafisa TEHAMA, Maafisa Rasilimali watu, Maafisa Mipango, Maafisa Mawasiliano, Wahasibu pamoja na Watumiaji wote wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini wanatarajiwa kushiriki.

Lengo la kikao kazi hicho ni kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao ili kujadiliana juu ya mafanikio, changamoto pamoja na kuweka mikakati mbalimbali ya kukuza Serikali Mtandao nchini ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika Taasisi za Umma; sambamba na

kuboresha utendaji kazi katika Taasisi hizo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Ndugu Wanahabari, Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ndiyo taasisi iliyopewa jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza juhudzi za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Taasisi za umma ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA yanazingatiwa katika Taasisi hizo.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka hushirikiana na wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao katika kukuza juhudzi za Serikali Mtandao nchini. Miongoni mwa juhudzi hizo ni pamoja na kukutana na wadau hao kupitia Vikao Kazi vya Serikali Mtandao vinavyoandalishi na Mamlaka.

Aidha, Kikao Kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kinaongozwa na kaulimbiu isemayo "**Mifumo Jumuishi ya TEHAMA kwa utoaji huduma Bora kwa Umma**" Falsafa ya Kaulimbiu hii ni kuhamasisha Taasisi za Umma kutumia mifumo jumuishi inayowasiliana katika utendaji kazi kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Ndugu Wanahabari,

Kwa ufupi nizungumzie baadhi ya mafanikio yatokanayo na Mamlaka ya Serikali Mtandao kuwa ni pamoja na;

- ❖ *Kusimamia uziangatiaji wa Sera, Sheria na miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma.*
- ❖ *Kuwezesha usanifu na ujenzi wa mifumo ya serikali mtandao ya kitaasisi na ya kisekta ili kuboresha utoaji huduma kwa Umma.*
- ❖ *Kuboresha na kuongeza mawanda ya kusimamia uendeshaji wa miundombinu shirikishi ya serikali mtandao.*
- ❖ *Kutoa msaada wa kiufundi kwa Taasisi za umma katika matumizi sahihi na salama ya huduma za Serikali Mtandao katika kuwashudumia wananchi.*

- ❖ *Kushirikiana na Taasisi za Umma na Taasisi Binafsi katika kuboresha utoaji huduma za Serikali kwa wananchi kupitia TEHAMA.*
- ❖ *Kusimamia na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya tafiti kwa ajili ya ubunifu katika serikali mtandao.*
- ❖ *Kusimamia utoaji wa mafunzo ya utekelezaji wa serikali Mtandao kwa watumishi wa umma*

Mamlaka imejipanga kuweka mwelekeo wa Serikali Mtandao katika miaka ijayo kwa kuanda na kutekeleza mikakati madhubuti ili serikali mtandao ifikie kuwa na:

- i. Sehemu moja ambayo huduma mtandao zote zitakuwa zinapatikana.
- ii. Uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka, hasa zile za akili bandia, sarafu za kidijiti na teknolojia za kifedha, ili kuwezesha maboresho ya kiutendaji katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma.
- iii. Na vijana wa kitanzania wenyewe uwezo mkubwa wa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao.
- iv. Uzalishaji wa vifaa na miundombinu ya TEHAMA (Hardware) ndani ya Tanzania
- v. Mifumo na miundombinu ya serikali mtandao ilio bora na imara zaidi.
- vi. Ubudilishanaji kamili wa taarifa miongoni mwa mifumo tumizi ya kitaasisi na kisekta ya serikali mtandao.
- vii. Uwezo mkubwa wa kudhibiti matishio ya usalama mtandaoni.
- viii. Na namba moja ya utambuzi kurahisisha utoaji wa huduma mtandao kwa umma.

Ndugu Wanahabari,

Mamlaka ya Serikali Mtandao inatoa rai na kuwakumbusha wadau wote wa TEHAMA hapa nchini kushiriki kikamilifu katika Kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kwa kufanya usajili kupitia mfumo wa TSMS (<https://tsms.ega.go.tz>)

ASANTENI

Imetolewa Na:

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz

“Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma”



MKURUGENZI MKUU
Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA)

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz

“Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma”

